# UMEUMBWA KWA KUSUDI

Gerhard Nehls

01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 1 01-11-2021 20:47:27

Original Title: Purpose & Aim

This is a publication of
Life Challenge © SIM 2021
P.O. Box 50770-00200,
Nairobi, KENYA
**info@lifechallenge.de**

All rights reserved. No part of this book may be reproduced without written permission, except for brief quotations in books and critical reviews.

Translation: John Augustine Mabutagulwa, Zanzibar, Tanzania

Printed and bound in Kenya

# Umeumbwa Kwa Kusudi

Si mengi katika maisha yanayoweza kulinganishwa na hisia ya mama kwa mtoto wake mchanga: hata awe mdogo kiasi gani, ni muujiza kamili kuanzia kichwani hadi kwenye vidole vya miguu. Mtu hataacha kufurahia vidole vidogo vichanga vikikumbatia kidole kimoja kikubwa alichopewa, akikishikilia kwa nguvu kadiri awezavyo. Hakuna kilichotengenezwa na mwanadamu kinachoweza kulingana na utendaji wa ajabu wa hiki kitoto kichanga - kila kitu kimeumbwa kwa kusudi.

Kusudi la kweli la cho chote kilichoundwa linaweza kuamuliwa tu na aliyekibuni na kukiunda, muumbaji wa hicho kitu. Kuhusu mwanadamu, mwumbaji ni Mungu peke yake! Bila shaka, mambo yanaweza kuondolewa kwenye kusudi lake la asili.

Kisu cha mkate kinaweza kuwa silaha ya kufisha.

Nguvu za atomu zinaweza kutumiwa kama nishati kwa ajili ya wanadamu au kwa kuwaangamiza wanadamu wao hao.

Maisha ya mtu anayetafuta kuishi sawasawa na kusudi alilolipanga muumbaji wake, ndiye aliye na kusudi sahihi katika maisha haya. Mtu kama huyo ana lengo lenye busara na uhalisi. Watu wengi wanalitambua hili. Kuna matatizo mawili tu husika. Itakuwaje mpango wa Mungu na makusudio yangu angalau hii sinapokubaliana? Watu wengi huamua kufanya ("mara hii moja tu") wafuate matamanio yao.



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 1 01-11-2021 20:47:27

Tatizo la pili ni gumu hata zaidi: Nitajuaje ni upi mpango wa Mungu na lengo lake kwa ajili ya maisha yangu? Ninawezaje kuwa na uhakika ni kitabu kipi kitakatifu ndicho ufunuo wa kweli kutoka kwa Mungu?

Kwenye mfuatano huu, kijitabu kingine JITAHIDI KULINGANISHA, kinachopatikana kwetu, swali hili linajibiwa kikamilifu.

Injili, yaani "HABARI NJEMA", huonyesha mtazamo wa Mungu kwa wanadamu. Mtazamo huu si mzuri - si bila ya sababu - maana tumejifunza kupitia machungu. Lakini pia Injili huonyesha njia ya kuondokana na machafuko, udanganyifu, kukosa kusudi, kukosa lengo, na wasiwasi. Hapa kuna muhtasari mfupi wa Injili ni nini.

## INJILI NI NINI?

Vitabu vingi vimeandikwa kujibu swali hili. Hebu tuangalie kimsingi. Baadaye unapaswa kuisoma na kuichunguza Injili wewe mwenyewe.

Maana ya "INJILI" ni "habari njema", Kuna aina nyingi za habari njema duniani, lakini katika Biblia ina maana tu kuwa ujumbe wake ni 'habari njema' kweli. Mungu amefungua njia ya kumpatanisha mwanadamu na yeye mwenyewe. Hili limeandaliwa hatua kwa hatua tangu mwanzo wa wanadamu. Hebu sasa tuwaangalie watu waliotajwa mwanzoni mwa Biblia.

## MAMBO YALIHARIBIKA

Mwanzoni mwanadamu aliishi kwa amani na umoja na uhuiano na Mungu. Kisha likaja anguko: Adamu (kwa Kiebrania ni "mwanadamu") na Hawa, wakisongwa na matamanio na vivutio vyao binafsi, walinuia kutimiza mapenzi yao wenyewe chini ya "uongozi" wa Shetani: Walitaka wawe kama Mungu. Kiburi na ufidhuli viliwafanya wawe waasi kwa Bwana wao. Matokeo yake, walifukuzwa waondoke kwenye bustani ya Edeni. Mara uzao wao ukafuata mfano wa wazazi wao na



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 2 01-11-2021 20:47:27

kuthibitisha upotovu wa mwanadamu anayeishi nje ya utawala wa Mungu. Mmoja alimwua ndugu yake mwenyewe.

Kuanzia hapo tunasoma kuhusu uasi na uovu wa wanadamu. Sote tumezaliwa na msukumo mkubwa ndani yetu wa kutenda dhambi. Hakuna mwanadamu aliyehitaji kufundishwa kutenda maovu. Kila mmoja amezaliwa na uwezekano wa tabia hiyo. Biblia inasema hivi:

> *BWANA akaona jinsi uovu wa mwanadamu ulivyokuwa mkubwa duniani, na ya kuwa kila mwelekeo wa mawazo ya moyo wake wakati wote ulikuwa mbaya tu.* (Mwanzo 6:5)

Hata hivyo, wanadamu, hadi siku hizi wanadamu - wamekataa uamuzi wa Mungu wakiona ni wa kupita kiasi. Wamechagua kuwa na hali ya kutarajia mazuri, wakiamini kuwa wanaweza kujiboresha wenyewe. Mungu kamwe hajashiriki mtazamo kama huo. Kwenye Agano Jipya tunasoma:

> *Kwa maana tunajua kwamba sheria* [amri za Mungu] *ni ya kiroho, lakini mimi ni wa kimwili* [yaani mwenye mawazo ya kimwili]*, nikiwa nimeuzwa kwenye utumwa wa dhambi.*
>
> *Sielewi nitendalo, kwa maana lile ninalotaka kulitenda, silitendi, lakini ninatenda lile ninalolichukia.*
>
> *... ninafahamu kwamba hakuna jema lolote likaalo ndani yangu, yaani, katika asili yangu ...*
>
> *Kwa kuwa nina shauku ya kutenda lililo jema, lakini siwezi kulitenda.*
>
> *Sitendi lile jema nitakalo kutenda, bali lile baya nisilolitaka, ndilo nitendalo.*
>
> *... Hivyo naiona sheria ikitenda kazi. Ninapotaka kutenda jema, jambo baya liko papo hapo.*
>
> *Kwa maana katika utu wangu wa ndani naifurahia sheria ya Mungu. Lakini ninaona kuna sheria nyingine inayotenda kazi katika viungo vya mwili wangu inayopigana vita dhidi ya ile sheria ya akili yangu. Sheria hii inanifanya mateka wa ile sheria ya dhambi inayofanya kazi katika viungo vya mwili wangu.* (Warumi 7:14-23)



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 3 01-11-2021 20:47:27

Ukiwa wewe ni mwaminifu, hujisikii kulazimishwa kuikubali kweli ya kauli hii? Kuitambua kweli hii ni hatua ya kwanza ya kupona kiroho! Udanganyifu mbaya zaidi ni kujilinganisha na wengine, tukaamua kuwa hata hivyo sisi si wabaya kiasi hicho. Hata hivyo tunapoitambua hali yetu mbele za Mungu, tunajaribu kuifidia kwa "majukumu" ya kidini na "matendo mema". Hata tunashikilia kuwa tunaweza kuifuta dhambi yetu.

Gharika kuu ilikuwa hukumu ya Mungu. Ni Nuhu na familia yake ya karibu tu waliopata *... kibali machoni pa BWANA...*

**Nuhu alitembea na Mungu**

*... Noa alikuwa mtu wa haki, na mkamilifu miongoni mwa watu ..., tena alitembea na Mungu.*
(Mwanzo 6:8-9)

Basi asili ya haki yake ilikuwa nini? Alikataa kushiriki katika dhambi akatii Neno la Mungu. Hii ndiyo maana ya imani.

## KUJENGA MINARA YA KUFIKIA MBINGU

Inasikitisha kusema, uzao wa Nuhu haukuwa bora kuliko wanadamu wa kabla ya gharika. Walifikiria mpango wao na kusema:

> *"Njoni, tufyatue matofali ..." Walitumia matofali badala ya mawe, na lami kwa ajili ya kushikamanishia... Ndipo wakasema, "Njoni, tujijengee mji wenye mnara ambao utafika hadi mbinguni, ili tujipatie jina ..."* (Mwanzo 11:3-4)

Kwa nini mtu huchoma matofali? Kuyafanya yawe imara yasiingiwe na maji. Kwa nini mtu atumie lami badala ya saruji? Huenda isiwe na nguvu kuzidi udongo, lakini tena maji hayawezi kupenya. Kwa nini mtu atake kujenga mnara wa kufika hadi mbinguni? Sababu moja inatolewa:

*"Ili tujipatie jina".* Inavutia kuwa Mungu alimwambia Ibrahimu mtumishi wake: *"Nitalitukuza jina lako..."* (Mwanzo 12:2)

Jina la Ibrahimu lina umuhimu, maana Mungu alilitukuza. Watu walitaka kujifanyia jina - ni nani anayewajua? Kuna jibu



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 4 01-11-2021 20:47:27

la pili ambalo ndilo msingi wa wao kuujenga mnara. Ilikuwa njia yao ya kuepuka uwezekano wa adhabu ya Mungu ya gharika jingine. Maji yakifurika tena kama matokeo ya kuasi kwao, wawe salama wakiwa juu ya huo mnara. Hivyo ndivyo walivyofikiria. Walipoujenga mnara (*"ambao utafika hadi mbinguni"*), tunasoma, na kuna kejeli:

*Lakini BWANA AKASHUKA ili auone mji na mnara.*
(Mwanzo 11:5)

Tangu wakati huo mwanadamu hujaribu kujenga 'minara' ili aiepuke hukumu ya Mungu - 'minara' ya kifalsafa, ya kisiasa, lakini iliyoenea ni 'minara' ya kidini. Hii ndiyo mifumo ya kidini inayoahidi kutukinga dhidi ya hukumu baada ya kushindwa kuishi inavyotaka sheria ya Mungu ya kutufanya tuwe na ushirika naye.

*"Mimi ndimi BWANA Mungu wako ...*

*Usiwe na miungu mingine ila mimi.*

*Usijitengenezee sanamu katika umbo la kitu chochote ...*

*Usilitaje bure jina la BWANA Mungu wako ..."*
(taz. Kutoka 20:1-7)

Kwa kuongezea kuna sheria zinazodhibiti mahusiano ya watu:

*"Waheshimu baba yako na mama yako, ... Usiue. Usizini. Usiibe. Usimshuhudie jirani yako uongo. Usiitamani ... chochote kile alicho nacho jirani yako."*
(taz. Kutoka 20:8-17)

Agano Jipya huiweka hivi sehemu ya mwisho:

*Upendo haumfanyii jirani jambo baya. Kwa hiyo, upendo ndio utimilifu wa sheria.* (Warumi 13:10)

Yuko wapi mwanaume au mwanamke mwenye upendo kama huo? Sawa, tunasema, "Ninakupenda!" Lakini tunakuwa na maana ya "Ninakutaka kwa faida yangu!"



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 5 01-11-2021 20:47:27

## MBINAFSI AU MTIIFU

Abramu, au kama alivyoitwa baadaye Abrahamu, aliishi kwenye jamii kama hii. Mungu alimwita atoke kwenye jamii yake na mazingira yake ya kidini - akatii. Wala hakuwa mkamilifu. (Mwanzo 12:10-20; 15:1-6 pamoja na 16:1-4; 17:15-19; 20:1-11 n.k.), lakini *akamwamini BWANA, naye kwake hili likahesabiwa kuwa haki.* (Mwanzo 15:6)

Abrahamu alimtii Mungu kwa kutii Neno lake, aling'ang'ania kwenye agano la Mungu. Kama ilivyo kwenye vitabu vya uhasibu pande mbili za kupokea na kutoa, kuna hesabu iliyotunzwa kwa ajili ya maisha ya kila mwanadamu. Kila dhambi - kupenda mtu au kitu fulani zaidi kuliko kumpenda Mungu, sikumpenda jirani kama ninavyojipenda mwenyewe (inabidi tulifikirie hili!), kushindwa ko kote kimawazo, kimaneno au kimatendo - huandikwa kwenye "kitabu" dhidi yetu. Na matendo yetu mema? Huonekana wapi? Hapa kuna habari mbaya: Kuyatekeleza hayo ni wajibu wetu!

Yesu alisema hivi:

*"... mkiisha kufanya mliyoagizwa, semeni, 'Sisi tu watumishi tusiostahili; tumefanya tu yale tuliyopaswa kufanya.'"* (Luka 17:10)

Kwingineko tunasoma kuhusu Ibrahimu:

*... imani yake na matendo yake vilikuwa vinatenda kazi pamoja, nayo imani yake ikakamilishwa na kile alichotenda.* (Yakobo 2:22)

Matendo kamwe hayawezi fidia dhambi.

Mfikirie mwuaji aliyeletwa mbele ya hakimu na akaonekana kuwa ana hatia ya mauaji. Baada ya mwendesha mashitaka kutetea dai lake na kuomba kuwa mtu huyu ahukumiwe kifungo cha maisha jela, hakimu akampa mshitakiwa nafasi ya mwisho ajitetee. Mshitakiwa anajitetea: "Mheshimiwa, ni kweli kabisa nimemwua mtu huyu, nina hatia. Lakini tafadhali, jaribu kutazama upande mwingine pia. Wakati wote nimemuheshimu mama yangu; Kwa miaka mitano sijakosa kwenda kazini; Wakati



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 6 01-11-2021 20:47:27

wote nimekuwa nikilipa kodi yangu ya mapato serikalini; hata nimewapa mkate na maziwa watoto wa mitaani, wakati wtu wengine wamepita tu bila kuwajali; Nimeishi kwa wiki kadhaa bila ya chakula wala kinywaji ili nijifananishe na maskini na wanaoteseka; kamwe sijawa na kiburi cha kunizuia kusali … Na nimefanya mema mengi zaidi katika maisha yangu ambayo sijakueleza. Huoni kuwa si haki kunihukumu kwa sababu ya hilo kosa moja nililofanya? Huwezi kukubali kuwa nimefanya mengi zaidi yaliyo mema kuliko mabaya?”

**Na matendo yetu mema? Huonekana wapi? Hapa kuna habari mbaya: kuyatekeleza hayo ni wajibu wetu!**

Hakuna hakimu mahali po pote duniani, anayeweza kuvunja sheria na aruhusu mtu kama huyo aachwe huru. Matendo mema hutarajiwa kutoka kwetu, lakini lazima tuwajibikie dhambi zetu.

Hata hivyo habari njema ni kuwa, ni imani ya Abrahamu iliyohesabiwa kwake kuwa ni haki:

> *Abrahamu akamwamini* B*WANA*, *naye kwake hili likahesabiwa kuwa haki.* (Mwanzo 15:6)

Katika Abrahamu na uzao wake Mungu alitaka kuwaonyesha wanadamu msingi wa kuishi naye, na kanuni yake ya upatanisho baada ya kuasi. Kwa uasi wa kukusudia au usio wa kukusudia tunatangaza vita juu ya Mungu. Tunakuwa waasi. Lakini Mungu anatupa amani!

Israeli walikuwa walete habari njema ya huyo Mungu mmoja na mpango wake kwa ajili ya mwanadamu kwenye ulimwengu uliokuwa gizani la dini iliyojengwa juu ya udanganyifu wa mwanadamu na mapepo. Lakini Israeli “walimsahau” Mungu wa Abrahamu wakaishi maisha bila Mungu.

Mungu aliingilia tena alipomtuma Musa. Waisraeli, wakiishi utumwani Misri, walikombolewa kwa ishara na maajabu yenye nguvu aliyofanya Mungu. Baadaye hakuna ambaye hakuutambua ukuu na uweza wa Mungu. Mungu alifanya agano na Israeli. Hili ndilo linaloitwa Agano la Kale. Mungu



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 7 01-11-2021 20:47:27

aliagiza kuwa Israeli ifuate njia mpya ya maisha. Alilitoa agizo lake kuu na kutamka:

*Tazama, naweka mbele yako leo uzima na mafanikio, mauti na maangamizo.*

*Ninakuamuru leo kwamba umpende* BWANA *Mungu wako, utembee katika njia zake, na kutunza maagizo yake, amri na sheria zake; ndipo utakapoishi na kuongezeka, naye* BWANA *Mungu wako atakubariki katika nchi unayoiingia kuimiliki.* (Kumbukumbu 30:15-16)

*Leo ninaziita mbingu na nchi kama mashahidi dhidi yako kwamba nimeweka mbele yako uzima na mauti, baraka na laana. Basi sasa chagueni uzima...*

*... upate kumpenda* BWANA *Mungu wako, uisikilize sauti yake na kuambatana naye. Na atakupa wingi wa siku ili upate kuishi katika nchi aliyoapa kuwapa baba zako Abrahamu, na Isaka na Yakobo.* (Kumbukumbu 30: 19-20)

## KUVUNJA AGIZO LA MUNGU

Lakini kitatokea nini mtu akivunja moja la maagizo hayo? Atakuwa amepotea?

*Kama kweli mnaitimiza ile sheria ya kifalme inayopatikana katika Maandiko isemayo, "Mpende jirani yako kama unavyoipenda nafsi yako," mnafanya vyema.*

*Lakini kama mnakuwa na upendeleo kwa watu, mnatenda dhambi, na sheria inawahukumu kuwa ninyi ni wakosaji. Kwa maana mtu yeyote anayeishika sheria yote lakini akajikwaa katika kipengele kimoja tu, ana hatia ya kuivunja sheria yote. Kwa sababu yeye aliyesema, "Usizini," alisema pia, "Usiue." Basi kama huzini lakini unaua, umekuwa mvunjaji wa sheria.* (Yakobo 2:8-11)

*Kama mtu katika jumuiya ametenda dhambi pasipo kukusudia na kufanya lile lililokatazwa katika amri yo yote ya* BWANA*, yeye ana hatia. Atakapofahamishwa dhambi*



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 8 01-11-2021 20:47:27

*yake aliyoitenda, ni lazima alete mbuzi jike asiye na dosari ... Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha sadaka ya dhambi na kumchinjia mahali pa kuteketezea sadaka.*

*Kisha kuhani atachukua sehemu ile ya damu ... na kuimwga damu … chini ya madhabahu. ... naye kuhani atayateketeza juu ya madhabahu kama harufu nzuri ya kumpendeza* Bwana*. Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake, naye atasamehewa.* (Walawi 4:27-31)

**Matendo kamwe hayawezi idia dhambi**

Mtu atapotea akivunja Sheria ya Mungu bila ya kutafuta upatanisho kwa njia ya sadaka - kulingana na maagizo ya Mungu! Lakini kwa nini Mungu alichagua njia ya kikatili hivyo - njia ya sadaka? Ninafikiri alitaka kuwadhihirishia watu uzito wa ubaya wa dhambi yao. Ikikulazimu kutoa sadaka tena na tena, kuchinja na kuteketeza mfugo wako unaoupenda kwa ajili ya dhambi unayoifanya - hakika utajizuia usiendelee kutenda dhambi. Mungu alitaka watu wake wajizuie na waishi kwa ajili yake yeye peke yake. Lakini kama watu walivyo, walinung'unika na kuasi, na hatimaye waliangukia kwenye ibada za sanamu na giza kamili. Mungu, pamoja na mpango wake mpya wa maisha, siyo tu aliachwa, bali alisahauliwa.

Maonyo yote ya Mungu yalikuwa ya kweli. Waisraeli waliishi maisha ya kushindwa na matokeo yake, ili unabii wa Mungu utimie, walitawanywa katika mataifa yote, wakiishi kwa mateso makubwa kwa karne nyingi.

Waisraeli kama wateule wa Mungu, walitengwa kwa sababu ya kutotii. Walikuwa wamelivunja "Agano la Kale". Hata hivyo, Mungu aliufuatilia mpango wake kwa wanadamu. Tayari Mungu alikuwa amewaambia Adamu na Hawa kuhusu mtu atakayetoka kwenye uzao wao, na "kuponda" kichwa cha shetani, huyu atoke kwenye uzao wa Ibrahimu, na Mungu anamwambia Ibrahimu:

*Na kupitia kwako mataifa yote duniani yatabarikiwa.* (Mwanzo 12:3)



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 9 01-11-2021 20:47:28

*Uzao wako utahesabiwa kupitia kwake Isaka.*
(Mwanzo 21:12)

## AHADI KUU: HUYO MASIHI

Wayahudi walimwita huyu mkombozi mtarajiwa Masihi wao (Mfalme-kuhani, au mtawala atawakilisha watu mbele za Mungu). Mungu alisema kuwa huyo lazima awe wa kabila la Yuda, wa uzao wa Daudi:

*Nimefanya agano na mteule wangu, nimemwapia mtumishi wangu Daudi, 'Nitaimarisha uzao wako milele na kudumisha ufalme wako kwa vizazi vyote.'* (Zaburi 89:3-4)

*Nitamteua pia awe mzaliwa wangu wa kwanza, aliyetukuka kuliko wafalme wote wa dunia. Nitadumisha upendo wangu kwake milele, na agano langu naye litakuwa imara ... kiti chake cha enzi kama mbingu zinavyodumu ... Mara moja na kwa milele, nimeapa kwa utakatifu wangu, nami sitamdanganya Daudi.* (Zaburi 89: 27-35)

*BWANA alimwapia Daudi kiapo, kiapo cha uhakika ambacho hatakitangua: 'Nitamweka mmoja wa wazao wako mwenyewe katika kiti chako cha enzi ...'* (Zaburi 132:11)

*... kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume, nao utawala utakuwa mabegani mwake. Naye ataitwa Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani.*

*Kuongezeka kwa utawala wake na amani hakutakuwa na mwisho. Atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi na juu ya ufalme wake, akiuthibitisha na kuutegemeza kwa haki na kwa adili, tangu wakati huo na hata milele.* (Isaya 9:6-7)

Kiti cha enzi cha Daudi cha duniani kilirithiwa na mwanawe - lakini ufalme huo ulikwisha kuharibiwa na kusahauliwa zamani. Kwa kuwa Mungu anazungumzia kiti cha enzi cha milele lazima alikuwa na jambo kubwa zaidi. Hakuna ufalme wa



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 10 01-11-2021 20:47:28

kibinadamu ambao ni wa milele. Anaweza kuwa nani mwana huyu anayezungumziwa na nabii (aliyezaliwa na bikira - Isaya 7:14)? Ni Yesu, Masihi: Anawezaje kuwa Mungu mkuu, Mfalme wa Amani? Itabidi jibu tumwachie Mungu. Lakini amani hii iko wapi - haki na adili iliyoahidiwa? Ufalme huu uko wapi? Yesu aliyajibu maswali haya kwa namna hii:

> *"Ufalme wa Mungu haujii kwa kuchunguza kwa bidii, wala watu hawatasema, 'Huu hapa,' au 'Ule kule,' kwa maana Ufalme wa Mungu umo ndani yenu."* (Luka 17:20, 21)

Raia wa Ufalme wa Mungu wana amani na Mungu. Wamesamehewa na kurudishwa kwa Mungu na wamepokea haki.

> *Nami nionekane mbele zake bila kuwa na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu kwa njia ya imani.* (Wafilipi 3:9)

Yesu alipozaliwa alitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliomlenga yeye. Alianzisha Ufalme wa Mungu. Mungu amejifunua ndani ya Yesu. Yesu aliishi maisha bila dhambi mbele ya ulimwengu uliokuwa ukimtazama. Akiwaonyesha wanadamu anavyotarajia Mungu sisi tuwe. Alikufa msalabani - akawa *Hiyo* Sadaka anayoihitaji kila mtu ili apatanishwe na Mungu Baba.

> *Yeye* [Kristo] *mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, ili tufe kwa mambo ya dhambi, bali tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa.* (1 Petro 2:24)

Hii ndiyo "HABARI NJEMA" au "INJILI." Bila ya hiyo hakuna anachoweza kufanya mwanadamu, isipokuwa kuishi kwa kulingana na maagizo ya "nafsi" yake " mtumwa wa dhambi." Yesu alipokuja kama ilivyotabiriwa, alibeba hatia na dhambi zetu. Aliteseka akiyabeba matokeo ya dhambi zetu. Haki ambayo ingetupiga mimi na wewe ilimpiga Yeye. Hata akasema:



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 11 01-11-2021 20:47:28

*“Mimi ndimi mchungaji mwema … nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo.”* (Yohana 10:14-15)

*“Kondoo wangu huisikia sauti yangu nami nawajua, nao hunifuata, nami ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakaye-wapokonya kutoka mikono yangu.”* (Yohana 10:27-28)

Hiyo ndiyo habari njema! Yote ambayo huwezi kuyafanya yamekwisha kufanyika kwa ajilli yako. Sasa unaweza kuishi maisha yako yote katika shukrani kwa Mungu, kisha akawa Mwokozi wako (Isaya 63:7-11). Maisha yako ni mali yake, na wewe, kama kondoo aliyepotea na baadaye akapatikana, uweze kuisikia sauti yake na umfuate katika Imani. Anajua walio wake, maana aliutoa uhai wake kama fidia (malipo ya kununua uhuru wa mtumwa) kwa ajili yao - na huwapa uzima wake mwenyewe ule wa milele. Hiyo ndiyo habari njema!

Lakini Yesu hakubaki mautini! Alifufuka kutoka wafu! Habari njema nyingine! Aliinuliwa juu mbinguni, ... na *yuko mkono wa kuume wa Mungu, naye pia anatuombea.* (Warumi 8:34)

Bado kuna habari njema zaidi! Au ni habari mbaya kwako? Atarudi tena - kuwahukumu kwa haki wote ambao hawakutaka kupiga magoti mbele zake (Wafilipi 2:9,10), au waliojiamini mno hata wasione haja ya msamaha wake. Lakini atakuja kuwafufua wote waliokufa miili, lakini wakaweka tumaini na imani yao katika Yesu!

## MUNGU ANAWEZA KUAMINIWA

Haya yote ni sehemu ya Agano Jipya. Yalitabiriwa katika Agano la Kale hivi:

*“Siku zinakuja,” asema BWANA, “nitakapofanya agano jipya na …* [watu]*. Halitafanana na agano nililofanya na baba zao ... kwa sababu walivunja agano langu, ...*

*Hili ndilo agano nitakalofanya ... Nitaweka sheria yangu katika nia zao, na kuiandika mioyoni mwao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. ... nitasamehe*



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 12 01-11-2021 20:47:28

*uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena."* (Yeremia 31:31-34)

**Amani na Mungu haitokei tu hivi hivi**

Yesu alipokufa msalabani, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, Agano Jipya liliidhinishwa na sasa ni halali maana lina sababu thabiti. Liko wazi kwa wote wanaopenda kupokea msamaha wa Mungu kwa dhambi zao, kwa njia aliyoifanya yeye, hadi Atakaporudi kuitangaza hukumu. Habari njema hitakuwa halali kwa wale waliouzuia upendo wa Mungu, au waliopendelea dini iliyoundwa na wanadamu.

Hata hivyo, amani na Mungu haitokei tu hivi hivi. Ingawa Yesu alikufa kwa ajili ya wanadamu wote kiuwezekano, wanaopokea msamaha na radhi hiyo ni wale tu walioikubali kikamilifu karama hiyo. Kwa hiyo ni wajibu wa kila mtu binafsi kuingia kwenye amani na Mungu. Wote tumeagizwa tufanye hivyo, maana Biblia Inasema:

*... Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao. Naye ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho.*

*Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Kristo, kana kwamba Mungu anawasihi kupitia kwa vinywa vyetu. Nasi twawaomba sana ninyi kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu.* (2 Wakorintho 5:19-20)

Kwa kweli tunaagizwa tumrudie Mungu:

*Zamani wakati wa ujinga, Mungu alijifanya kama haoni, lakini sasa anawaamuru watu wote kila mahali watubu.*

*Kwa kuwa ameweka siku ambayo atauhukumu ulimwengu kwa haki ...* (Matendo 17:30, 31)

Kwa hiyo, ili tusamehewe na kukubaliwa, lazima tukubali mwito huu na agizo hili.



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 13 01-11-2021 20:47:28

## KUSAMEHEWA MILELE

Hili hutokea unapoyachunguza maisha yako, unapoitambua dhambi iliyomo, unapoikiri kwa Mungu, kuijutia na kuiacha na ukamwomba Yesu akusafishe, akukubali na awe Bwana wa maisha yako.

*Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka kwake na kuwatangazia ninyi: kwamba Mungu ni nuru na ndani yake hamna giza lolote. Kama tukisema kwamba twashirikiana naye huku tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatutendi lililo kweli.*

*Lakini tukienenda nuruni, kama yeye alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*

*Kama tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo ndani yetu.* (1 Yohana 1:5-8)

*Kama tukisema hatukutenda dhambi, twamfanya yeye kuwa mwongo na neno lake halimo ndani yetu.*
(1 Yohana 1:10)

Akiyajibu haya, Mungu alijitolea mwenyewe akisema:

*"... nitasamehe uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena."* (Yeremia 31:34)

Wasomaji wa Kiislamu watachukizwa na msemo wa "Mwana wa Mungu". Lazima ijulikane kuwa Biblia haiutumii msemo huu kuonyesha kuwa Mungu alikuwa na "uhusiano" na Mariamu uliosababisha kuzaliwa kwa Yesu. Msemo huu unatumika kama mfano tu.

Kwa kuwa ni sadaka ya Yesu pekee yake inayoweza kutusafisha na kutuweka huru kutoka dhambini, tunampokea Yesu kama Wokovu wetu (Kiebrania: 'Yeshua' = Yesu). Huu ndio mwanzo wa maisha ya umoja na Mungu. Sasa utakuwa umesafishwa. Uchafu wa maisha yako na moyo wako umeondolewa. Sasa maisha yako lazima yajazwe mambo mapya, lakini kwanza lazima ajazwe na Mungu mwenyewe. Lazima aruhusiwe na



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 14 01-11-2021 20:47:28

akaribishwe (kwa maombi) ili aketi kwenye kiti cha enzi cha maisha yako na akae moyoni mwako. Roho Mtakatifu wa Mungu ataanza kuyafanya upya maisha yako. Mapenzi yako yakisalimu amri kwenye mapenzi Yake.

*Naye alikufa kwa ajili ya watu wote, ili kwamba wote wanaoishi wasiishi tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa na kufufuliwa tena kwa ajili yao.* (2 Wakorintho 5:15)

**Tumerudishwa kwenye asili na maana ya maisha**

*Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya. Haya yote yanatokana na Mungu, ambaye ametupatanisha sisi na nafsi yake kwa njia ya Yesu Kristo na kutupata sisi huduma ya upatanisho.* (2 Wakorintho 5:17-18)

Mtu aliyefanya jambo hili huwa mali ya Mungu. Anakubaliwa na Mungu kwa masharti yake Mungu, amesamehewa. Sasa yeye hupokea mamlaka mapya na mwongozo katika Neno la Mungu, kwa anaishi maisha mapya. Ni kwa utukufu wa Mungu na kwa kuanzisha Ufalme wake duniani. Hili litaleta maisha mazuri na matakatifu. Tumerudishwa kwenye asili na maana ya maisha - maisha ambapo utimilifu wote wa Mungu, sio tu ule wa kiroho, bali pia yaliyokusudiwa katika uumbaji. Tunaweza kuishi maisha haya kila siku. Huenda la muhimu kuliko yote ni: Ninaweza kuyajua majaliwa yangu. Hakuna hofu tena kwa yajayo, hasa kifo, maana dhambi zangu zimesahauliwa na Mungu. Anasema hivyo! Na *Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu.* (Warumi 8:1)

Kama tu Nuhu na familia yake walivyokuwa salama ndani ya Safina, kadhalika, wale *walio ndani ya Kristo Yesu* wako salama mbali na hasira ya Mungu inakayokuja. Haki ya Mungu imeridhishwa, maana dhambi zetu zote zimeadhibiwa ndani ya Yesu.

Maisha haya mapya huleta matamanio mapya:

- Kwanza, kuishii maisha ya kumpendeza Mungu katika kujitoa na shukrani katika upendo.
- Pili, hamu ya ushirika na watu wenye mawazo kama hayo.
- Na tatu, kuwashirikisha wengine tumaini na maisha haya mapya. Kwa kweli hilo ndilo kusudi la kitabu hiki.

Kwa hiyo tunakukaribisha usione aibu, usingoje tu ukisubiri wakati mwingine, bali wasiliana nasi kwa taarifa zaidi, au kwa majadiliano kuhusu mada za kijitabu hiki, wala usijisikie kuwa unawajibishwa kuendelea zaidi kuliko vile unavyotaka. Mawasiliano yote hayatahusisha mtu mwingine.

Ukipenda kuwasiliana nasi, tuandikie ukitumia anuani iliyo karibu zaidi na wewe, kulingana na anuani zilizo mwisho wa kijitabu hiki. Tumia anuani iliyo nyuma ya kitabu hiki.



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 16 01-11-2021 20:47:28

**Maswali**

Maswali yafuatayo yatakuwa na faida kubwa kwa kuufahamu zaidi ujumbe wa kijitabu hiki. Tafadhali tuma majibu yako na utujulishe ni kijitabu kipi kingine utapenda kupokea kutoka kwenye mfuatano huu.

1. Elezea Uislamu unavyotarajia kwa wafuasi wake kutimiza desturi za dini.
2. Habili alionyeshaje imani ya kweli kwa Mungu?
3. Ikamilishe sentensi: “Na Ibrahmu alimwamini Bwana; na Bwana ……….. …… …. ………………… kwa sababu ya imani yake.”
4. Eleza tofauti ya msingi kati ya jua na mwezi.
5. Toa mfano wa jinsi Mungu alivyomsikiliza Ibrahimu.
6. Musa aliuakisi vipi utukufu wa Mungu?
7. Ikamilishe sentensi: “Dhabihu inayokubaliwa na Mungu ni roho iliyovunjika; … ………… ……… ………….. …………………….. …………….. ……..” Eleza kwa maneno yako mwenyewe hili lina maana gani kwako.
8. Ni vingapi kati ya vitabu 39 vya Maandiko ya Wayahudi yanayojulikana kama Agano la Kale katika Biblia hutoka kwenye wakati wa manabii Yeremia na Ezekieli?
9. Ilibidi Yohana Mbatizaji (Yahya) aseme nini kuhusu Yesu kinachoelezea kazi yake maalum?
10. Una jibu gani kwa swali: Kuna zawadi gani ya thamani kuliko zote aliyowahi kukupa Mungu? Ni zawadi gani iliyomgharimu kuliko zote?
11. Elezea kwa kifupi tofauti: “Malaika ni …….. …………………….. ……………., Watu wa Mungu waliokombolewa ni ………. …………. …………. ……………………..”

Tafadhali tutumie majibu yako pamoja na maswali au masuala yo yote unayopenda kujadili. – Umeliona hili kwenye maisha yako mwenyewe? Au kuna njia tunaweza kukusaidia?

Asante.



01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 17 01-11-2021 20:47:28

**Vijitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya wasomaji wetu:**

1. Umeumbwa kwa Kusudi
2. Jitahidi Kulinganisha
3. Mwisho Usiojulikana
4. Mpendwa Abdallah
5. Mtu mwenye Ujumbe
6. Kwa nini Kuiamini Biblia
7. Kurani na Biblia
8. Fuata Moyo wako

Al-Kitab - *Kitabu cha Vitabu* (Kozi ya Biblia)

*Tafadhali nitumie* ....................................................................
.........................................................................................
.........................................................................................
.........................................................................................

Tuma barua yako kwa:


**Hamasa ya Milele**
S.L.P. 11795
Arusha, TANZANIA
hymilele@gmail.com

**Life Challenge**
S.L.P. Box 50770- 00200
Nairobi, KENYA
info@lifechallenge.de




01MadeForPurpose-Swahili -Edited by SB.indd 18 01-11-2021 20:47:28